

# Msaada wa Kifedha katika Swedish

## Financial Assistance at Swedish (Swahili)

Swedish Health & Services inajali watu na mahitaji ya afya zao bila kujali wanaweza kulipa au hawawezi. Tufanya kazi na wagonjwa wetu katika masuala yoyote ya kifedha, ikiwa ni pamoja na kutafuta njia za kufanya huduma za matibabu kuwa rahisi. Hospitali za Swedish zinatoa msaada wa kifedha kwa wagonjwa ambao hawawezi kulipia gharama za matibabu yao. Kama unapata shida kulipia baadhi au huduma zako zote za afya, tafadhali Zungumza na Wakili wa Masuala ya Kifedha ya Mgonjwa au Mhudumu wa Huduma kwa Wateja kuona jinsi tunavyoweza kukusaidia.

**Nini ambacho kinajumuishwa?** Kwa huduma za dharura na ambazo ni za lazima kitabibu katika Hospitali za Swedish tunatoa msaada wa kifedha kwa wagonjwa wenye sifa, kwa kiwango cha ada kidogo, ikiwa na punguzo kuanzia 30 hadi 100% kulingana na uwezo wa kulipa. Msaada wa kifedha kwa huduma ambazo si za dharura na ambazo ni za lazima kitabibu au huduma zinazotoewa *nje* ya hospitali unategemeana na sera za kliniki au ofisi iliyokupatia huduma hiyo.

**Jinsi ya kutuma maombi?** Mgonjwa yeyote anaweza kuomba msaada wa kifedha. Mgonjwa anayehitaji msaada wa kifedha ni lazima atoe taarifa na nyaraka alizombwa katika maombi, isipokuwa ikiwa imesemwa vinginevyo. Fomu ya maombi inaweza kuagizwa kwa kupiga simu au kuchapwa kutoka kwenye tovuti ifuatayo.

[www.swedish.org/patient-visitor-info/billing/financial-assistance](http://www.swedish.org/patient-visitor-info/billing/financial-assistance)

**Maeneo Mengine ya Msaada wa Kiafya:** Ikiwa huna bima ya afya, unaweza kuwa na sifa kwa ajili ya programu nyinginezo za serikali na jumuiya. Tunaweza kukusaidia kuelewa ikiwa programu hizi (ikiwa ni pamoja na Medicaid na Apple Health) zinaweza kutosheleza gharama zako za matibabu. Tunaweza pia kukusaidia kutuma maombi kwa ajili ya hizi programu.

**Punguzo kwa wasiokuwa na Bima:** Swedish inatoa punguzo kwa wagonjwa wasiokuwa na bima ya afya. Tafadhali wasiliana nasi ikiwa una maswali kuhusiana na programu yetu ya punguzo la bei.

**Mipango ya malipo:** Malipo yoyote unayodaiwa yanaweza kulipwa katika moja ya njia zifuatazo: mpango wa malipo, fedha taslimu, hundi, malipo ya mtandaoni au kwa kutumia kadi. Ikiwa unataka mpango wa malipo, tafadhali piga namba kwenye bili yako kwa ajili ya msaada.

**Huduma ya Dharura:** Hospitali za Swedish pamoja na idara za huduma za dharura kwa hali za ugonjwa wa dharura (kama ilivyofafanuliwa na Sheria ya Matibabu ya Dharura na Kazi) bila ubaguzi kwa kadri ya uwezo wao, bila kujali iwapo mgonjwa ana uwezo wa kulipa au ana sifa za kupewa msaada wa kifedha.

### Wasiliana Nasi kwa Msaada wa Kifedha au Maombi

Kwa taarifa zaidi juu ya kupata msaada wa gharama zako za matibabu za Swedish, tafadhali piga simu katika Timu ya Huduma ya Wateja au mtembelee Wakili wa Masuala ya Kifedha ya Mgonjwa katika hospitali ya Swedish iliyopo jirani nawe. Tunaweza kukupatia fomu zozote unazotaka na tunaweza kukusaidia kutuma maombi kwa ajili ya msaada. Wagonjwa wanashauriwa kuomba msaada wa kifedha kabla ya kupokea matibabu, ikiwa tu inawezekana. Wagonjwa wanaweza pia kuomba kwa ajili ya msaada wakati wowote huku wakiwa wanapata matibabu na kwa kipindi cha muda baada ya kupata bili ya kwanza. Ikiwa una maswali au ungependa kupata fomu ya msaada wa kifedha, tafadhali wasiliana:

- Kwa simu: 877-406-0438
- Kwenye tovuti yetu: [www.swedish.org/patient-visitor-info/billing/financial-assistance](http://www.swedish.org/patient-visitor-info/billing/financial-assistance)